# Itikadi katika Riwaya za Awali za S.A Mohamed

Murithi Joseph Jesee

## Ikisiri

Wahakiki wengi wanapozungumzia msimamo na mielekeo ya mwandishi kuhusu maisha na ulimwengu uliomzunguka, huchukulia kwamba msimamo huu ni mmoja na tengemano. Ni kama kwamba mtunzi huongozwa na itikadi moja ambayo ni imani yake inayosawiri mtazamo wake kuhusu jamii katika kazi yake. Makala hii inanuia kuonyesha kuwa itikadi ni dhana badilifu na nyumbufu kulingana na namna mtunzi anavyowasilisha kazi yake, masuala makuu anayojadili, anavyosawiri wahusika wake, na mtindo mzima wa kazi yake. Itikadi ndiyo huelekeza misimamo, mielekeo na imani ya mtunzi na hivyo kuathiri mtazamo wa mwandishi kuhusu ulimwengu unaomzunguka ambao huweza kubadilika. Ni katika mkabala huu ambapo makala hii inalenga kutathmini namna itikadi katika riwaya za awali za S.A Mohamed ambazo zinawakilishwa na *Asali Chungu* (1978) na *Kiza katika Nuru* (1986) zinavyojitokeza ili kudhihirisha itikadi na dhana badilifu na nyumbufu na hivyo msimamo wa mtunzi huwa changamano wala sio mmoja na tengemano kama inavyofikiriwa na wahakiki wengi wa fasihi. Aidha, tutaonyesha kuwa itikadi ina mielekeo tofauti kwani itikadi ya mtunzi na itikadi tawala huweza kuwa tofauti.

## 1.0 Utangulizi

Miongoni mwa wasomi wa mwanzo kutumia dhana ya itikadi ni Cabanis Destute de Tracy ambaye ni mwanafalsafa kutoka Ufaransa. Aliibuni dhana hii mwaka 1796 kumaanisha mfumo wa fikra fulani au sayansi ya mawazo (Wamitila, 2008). Dhana hii ni changamano na imeleta mijadala mingi kati ya wasomi tofauti. Ni dhana ambayo ni telezi kuelezea kwa sababu ya sifa yake ya kuweza kufasiriwa kwa njia mbalimbali kutegemea malengo na dhamira ya yule anayeitumia (Chuachua, 2011:8). Kwa mujibu wa makala hii tutatumia itikadi kwa kuzingatia mikabala mitatu. Mikabala itakayotumiwa itajumuisha ule wa Karl Marx (1973) ambao unachukulia itikadi kama ung'amuzi potoshi, mkabala wa Louis Althusser (1981) unaochukulia itikadi kuwa jumla ya dhana za kitamaduni ambazo hutawala watawaliwa kupitia vyombo vya serikali na vya kiitikadi na kuchukulia kama udhahiri, na mkabala wa Antonio Gramsci (1985) unaoelezea itikadi kuwa ni mfumo wa mawazo ya tabaka tawala ambayo huendelezwa kwa ukubalifu na ukawaida.

Kwa jumla itikadi huwa ndio msingi unaomwelekeza msanii katika kuwasilisha ulimwengu wake kwa jamii lengwa kupitia maudhui anayojadili, dhamira zake, wahusika aliochagua na namna anavyowasawiri na mtindo aliotumia. Ni mawazo, mafunzo na malengo ya mtunzi yanayosawiri utekelezaji wa majukumu ya kidini, kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa ujumla wake. Ni mawazo ambayo humwongoza kila mtu duniani katika kutenda anayotenda na jinsi anavyotenda na humsaidia kuamua atekeleze yapi, aache yapi, ayatekeleze vipi na hivyo kuhalalisha ama kuharamisha matendo yote anayoyafanya (Rossiland, 1990).

Katika makala hii tunamwangazia S.A Mohamed, mtunzi ambaye ameandika riwaya, tamthilia na ushairi na makala nyingine nyingi. Tunaangazia riwaya zake *Asali Chungu* na *Kiza katika Nuru* kama kiwakilishi cha riwaya zake za awali ili kubainisha itikadi zinazojitokeza humo. Na ili kuonyesha kuwa msimamo na mwelekeo wa mtunzi sio mmoja na tengemano bali ni changamano zaidi kuliko ilivyofikiriwa awali. Katika kujadili mada hii tunaongozwa na nadharia mbili ile ya udenguzi na ile ya kimaadili. Kwa ujumla mihimili ya Nadharia ya Udenguzi inaweza kuelezwa kuwa maana za matini katika lugha ni nyingi kwa kufuata utaratibu wa umuundo wa kiashiria na kiashiriwa. Aidha, maana za matini huahirishwa na hivyo maneno na dhana hazina maana thabiti hivyo ni telezi. Pia, nadharia hii inaona kwamba uainishaji wa dhana zote kiulimwengu huzingatia uwili kama vile mke-mume, kizuri-kibaya na kilicho hai-kisicho hai. Kwa hivyo dhana zinazokinzana zinakaribiana kimaana. Hii inamaanisha kuwa maana za lugha sio thabiti; huelea juu ya maneno, maneno na matini hujengana na kupingana zenyewe na hivyo matini huwa na mielekeo mingi ya maana na huibua fasili nyingi; maana haipatikani katika ishara moja pekee lakini huwa katika hali ya kuwapo na kutokuwapo-mara imo mara haimo (Derrida, 1976). Kwa hivyo, nadharia hii inatupa fursa katika makala hii kutoa fasili nyingi za dhana ya itikadi katika riwaya za S. A. Mohamed.

Kwa upande mwingine Nadharia ya Kimaadili iliasisiwa na wanafalsafa Plato na Aristotle na kuendelezwa na Kant, Rousseau, miongoni mwa wengine (Hough, 1966). Aidha, watunzi wa Kiafrika kama Ngugi wa Thiong'o na Chinua Achebe wamezingatia nadharia hii katika kazi zao (Achebe, 1988). Nadharia hii hueleza kuwa fasihi ni zao la jamii na hutoa mifano ifaayo ya maadili kwa wakati maalum. Mazingira ya mtunzi kijamii na kihistoria huathiri kazi yake, fasihi ni kielezo cha maadili ya jamii kwa wakati maalum na mtunzi lazima azingatie maadili ya jamii kwa wakati wake ili kazi yake iwe faafu kwa jamii yake. Hivyo, Nadharia ya Kimaadili tumeitumia ili kubaini kuwa mtunzi hana budi kuibadilisha mitazamo, mielekeo na mafunzo yake kwa jamii kwani mtunzi ni kama mwalimu wa jamii yake.

## *2.0 Muhtasari wa Riwaya za* Asali Chungu *na* Kiza katika Nuru

Riwaya ya *Asali Chungu* inamhusu Zuberi ambaye ni mkuu wa wilaya na anamiliki mashamba makubwa. Zuberi na mkewe aitwaye Amina wanaishi maisha ya raha na starehe huku wanyonge kama Dude, Baya na Shaaban Supu, kati ya wengineo wakiishi kwa ufukara mkubwa. Bwana Zuberi anakosa kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi wanaoleta malalamiko kwake; kazi yake ni kuwafuata wasichana kwa raha na starehe. Mzee Zuberi anamnajisi Semeni mfanyakazi wake wa nyumbani ambapo Dude anazaliwa.

Dude anaishi katika mazingira duni na kukua akiona uasherati waziwazi kutoka kwa walezi wake, jambo linalompelekea kuwa mwasherati mkubwa na baadaye kuwa mpenzi wa siri wa Amina, mkewe Zuberi. Dude baadaye anakosana na Amina kwa sababu ya kutumia gari lake kumpeleka Baya hospitalini. Baadaye, Dude anapendana na Shemsa, bintiye Zuberi na Amina, na Amina anakuwa na msimamo kuwa Dude hamwoi Shemsa kamwe. Anasema hivyo ili kuepuka aibu ya vitendo alivyotenda hapo awali akiwa na uhusiano wa kimapenzi na Dude.

Mwishowe, Shemsa na Dude wanaoana na kuishi pamoja. Licha ya kuwa walipendana kwa dhati, Dude anampachika mimba Latifa dadaye Shemsha alipoenda kukaa kwao ili kuwasaidia. Hapo awali alikuwa ameapa kuwa mwaminifu kwa mkewe na kutohusika katika uasherati kamwe. Mwishoni mwa riwaya tunaona mapinduzi yakifanyika ghafla. Hii inatokana na ukandamizaji unaopelekea kuwako kwa mfumo wa kimwinyi ulioenea katika jamii hii. Maskini wanadai haki yao na wanatekeleza maafa kama vile kuichoma nyumba ya Mzee Zuberi na Bi Amina. Hii inaashiria mwisho wa umwinyi na mwanzo wa jamii mpya au ujamaa wenye usawa na haki kwa kila kiumbe. Dude, Shemsha na mtoto wao pamoja na Latifa wanaokoka. Hawakuangamia ilhali Amina na Binti Daudi waliangamia. Naye Zuberi alikuwa ameaga dunia hapo awali kutokana na maradhi ya moyo.

Kwa upande wake, riwaya ya *Kiza katika Nuru* inaanza na ugomvi baina ya Bwan Juba na Mvita ambao ni mtu na mwanaye. Bwan Juba pia ni bosi wake kazini. Hali hiyo inasababisha Mvita pamoja na Salma mchumba wake kufutwa kazi. Juba pia anamfukuza Mbishi mwanawe wa pili nyumbani baada ya mabishano kwa kumchora ukutani. Bwan Juba ana wake wawili ambao ni Kudura na Bi Khalitty, lakini amemtelekeza Kudura na anashughulika zaidi Bi. Khalitty. Kudura analazimika kukopa ili angalau kumwandalia mumewe Juba chakula anapokwenda kumtembelea. Mvita anapofutwa kazini anafanya kazi za chini jambo linalompa nafasi ya kutangamana na watu wa tabaka la chini na anaanza juhudi za kuwazindua. Anaenda kumtembelea mamake mara moja moja na kujaribu kumzindua aweze kutetea haki zake. Baadaye Kudura anazinduka hasa kutokana na kushuhudia Biti Japu akipigana na muuza nyama alipokataa kuwauzia nyama na kuwauzia watu mashuhuri kama Shehe. Bwan Juba anapomtembelea Kudura anamwandalia chakula lakini Juba anamtusi ndipo Kudura anaporudi jikoni na pauro tayari kukabiliana na mumewe ili autetee ubinadamu wake. Hata hivyo anazuiwa na marafiki wa Bwan Juba, Mzee Hussein na Mzee Kidambwe.

Baadaye Bwan Juba anamfukuza Kudura nyumbani na anakwenda kuishi na watoto wake. Mvita anafanya juhudi kuwazindua wafanyakazi na wananchi na wanapofanikiwa, Juba anaogopa na kumuua kwa kumtumia Shazia. Baadaye, Kudura na Mbishi wanamuua Juba kwa ushirikiano na Kitwana na Baker, lakini wanafikishwa mahakamani pamoja na Salma kwa mashtaka ya mauaji. Salma (mchumba wa Mvita) anashitakiwa kwa mauaji ya Mvita naye Mbishi na Kudura

wanashitakiwa kwa mauaji ya Bwan Juba. Kudura anajiua akiwa gerezani lakini kuna matumaini kwamba Salma ataachiliwa huru kwa sababu ana mimba ya Mvita (pia Mvita aliuawa na Shazia si Salma). Kuna matumaini kwamba kizazi kipya kitazaliwa kuendeleza harakati za kupigania haki na usawa hasa kupitia kwa barua anayopata Salma akiwa gerezani kuwa watu wanamngojea aachiliwe ili waendeleze harakati za kutetea maslahi yao. Kwa ujumla wahusika wa tabaka la juu kama Bwan Juba, Bw. Fadhili na Bw. Mtoro wanafaidika na mambo kama yalivyo na hawataki mabadiliko ya mfumo wa utawala ulioachwa na wakoloni, yaani utabaka una nguvu hata kuliko familia.

## *3.0 Itikadi katika Riwaya ya* Asali Chungu *na* Kiza katika Nuru

### *3.1 Itikadi katika* Asali Chungu

Katika riwaya hii, itikadi ya kimwinyi ndiyo inayodhihirika zaidi kama iliyotawala katika jamii hii. Imejitokeza kwa vigeu[1] kama mfumo wa kiuchumi, matabaka, elimu, utamaduni, dini, uchawi, asasi za utawala na nyinginezo. Katika riwaya hii mfumo wa kiuchumi unaojitokeza ni wa kimwinyi ambapo watu wachache humiliki nyenzo za uzalishaji mali kama vile mashamba makubwa huku wengi wakibakia maskini bila mashamba na kuwa wachochole na watumwa. Mfumo wa kimwinyi unajitambulisha kwa ubadhirifu na ufujaji wa mali miongoni mwa tabaka tawala. Kwa mfano, Zuberi na mkewe Amina wanaishi katika nyumba ya kifahari na wanamiliki mashamba makubwa na magari ya kifahari. Wanyonge kama Semeni, Dude, Bushiri, Mzee Omari kati ya wengineo wanaishi katika mazingira duni, wanavaa mavazi duni na kula vyakula vibaya, na hivyo wako radhi kufanya chochote ili waweze kujikimu kimaisha. Mfumo huu unatumiwa kuhalalisha vitendo viovu vya kina Zuberi na Amina kuishi kwa ubadhirifu na starehe. Nao kina Dude na Bushiri wanatumia sababu za mfumo huu wa uchumi kuhalalisha matendo yao ya wizi na uasherati na wanashindwa kuelewa hali yao hasa imesababishwa na nini na wanaweza kujinasua vipi na hivyo kudhihirisha kuwa mfumo wa kiuchumi ni kigeu kinachotumiwa kuhalalisha vitendo vya wahusika na hivyo ni kigeu cha kiitikadi kama Marx (1973) anavyosema.

Jamii ya *Asali Chungu* imegawanyika katika matabaka. Mtunzi anaonyesha kuwa utabaka umekithiri kwani matajiri wa tabaka la juu wanapata kila kitu wanachokitaka ilhali watu wa tabaka la chini wana matatizo chungu nzima. Mtunzi anaonyesha utabaka huletwa na mfumo wa kiuchumi. Zuberi ana shamba kubwa ambalo linatoa mazao mengi na kwa hivyo kumuweka katika tabaka la juu pamoja

---

[1] ni asasi au mifumo inayotumiwa kuendeleza itikadi tawala.

na mkewe Amina. Nyumba yao ni kasri kubwa ambalo limejaa vitu vya thamani. Kwa upande mwingine, kina Semeni, Dude, Bushiri na wengine wanaishi katika tabaka la chini. Hawa hawana vitu vya kimsingi kama chakula na elimu. Kwa hivyo tabaka ni mojawapo ya vigeu vya kiitikadi kwani hutumiwa kuhalalisha matendo ya wahusika yaani kina Zuberi na Amina waendelee kuishi kwa raha na starehe, nao kina Dude, Bushiri kati ya wengineo waishi kimaskini. Aidha, wahusika wanaofanya maovu kama Dude wanatumia utabaka kuhalalisha vitendo vyao viovu kwani wanataka pia kuwa katika tabaka la juu hivyo wako radhi kushiriki uasherati na kina Amina almuradi wajihisi kuwa ni wa tabaka la juu hivyo utabaka ni kigeu cha kiitikadi. Ninamaanisha kuwa kutokana na mfumo mbaya wa kiuchumi jamii ya *Asali Chungu* imegawika katika matabaka ya juu na ya chini. Kila tabaka linatumia utabaka wao kuhalalisha vitendo vyao na hivyo kuwa asasi au njia mojawapo ya kuendeleza itikadi ya kimwinyi.

Katika itikadi ya kimwinyi, elimu ni asasi inayotumiwa kuendeleza kizazi cha mabwenyenye. Mtunzi anaonyesha namna ambavyo elimu ni muhimu katika maisha kwani ilitumiwa kuwaweka watu katika matabaka mbalimbali. Mohamed anaeleza jinsi masomo ya Dude yanavyokatizwa akiwa darasa la sita kwa sababu ya ukosefu wa karo. Hii inaleta kuwapo kwa matabaka katika jamii kwa sababu ya ukosefu wa ajira inayotokana na elimu duni. Kwa upande mwingine watoto wa matajiri walipata elimu ya juu hata kuwenda ng'ambo kusoma. Shemsha mtoto wa Zuberi na Amina wanasomea ng'ambo na kufaulu katika masomo yao. Mtunzi anaeleza kuwa haya yote yanasababishwa na mfumo wa uzalishaji mali wa kimwinyi kwani waliopendelewa na mfumo huu ndio walioendelea kielimu. Hii inadhihirisha mtazamo wa Althusser (1981) kuhusu itikadi kuwa elimu ni kigeu kimojawapo cha kuendeleza itikadi tawala ambapo huwatayarisha watu kutekeleza majukumu tofauti katika jamii na kuwaweka katika matabaka fulani katika jamii na hivyo kuendeleza itikadi tawala.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mfumo wa kuumeni unajitokeza na kudhihirika zaidi kutokana na mfumo wa utawala wa kimwinyi uliodhihirisha ubozi na mamlaka. Jinsi ya kiume inatajwa kwa majina ya heshima na cheo kama vile Bwana Mkubwa, Bwana DC (uk. I) lakini kwa upande mwingine, mwandishi anasawiri wahusika wa kike akitumia majina ya kuwadunisha na kuwadharau kama vile Bi. Kikongwe na janajike kuwarejelea wanawake (uk. 1). Aidha, mwanamke anasawiriwa kama mtu asiyekuwa na haki ya kumiliki chochote. Katika mfumo huu mwanaume ndiye mmiliki wa mashamba na mali; hata mwanamke anaonekana kuwa ni sehemu ya mali yake. Aidha, mfumo wa kuumeni ni mojawapo tu ya vigeu vya itikadi kuu ya kimwinyi ambapo unahalalisha anasa, ubadhirifu wa mamwinyi na kusawiri mwanamke kama sehemu ya mali ya mwanamume ambayo inapaswa kuchangia katika starehe na ubozi wake. Mwanamke anapokataa nguvu hutumika kama vile Zuberi alivyomnajisi Semeni.

Katika riwaya ya *Asali Chungu* ndoa inasawiriwa kama asasi ya unyanyasaji na inatumiwa kuhalalisha itikadi kuu tawala ya kimwinyi kwa kuhalalisha ubozi na kuhodhi mamlaka na maovu mengine, kama ambavyo Althusser (1981) anavyosema kuwa ndoa na familia hutumiwa kuhalalisha itikadi kuu tawala. Aidha, dini ni asasi mojawapo ya kitawala ambayo huweza kutumiwa kuwapumbaza wanyonge wasione ukweli. Kwa mujibu wa Marx na Engels (1973) katika *On Literature and Art,* dini hutumiwa kueneza itikadi za uongo za tabaka tawala ili liendelee kudhibiti mamlaka ya utawala na nguvu za kiuchumi. Hufanya hivi kwa kueneza dhana ya majaliwa kumaanisha kuwa Mungu ameratibu maisha ya wanadamu na yote wanayopitia ni mpango wa Mungu. Hii humaanisha kuwa kama wao ni maskini huona kuwa ni mapenzi ya Mungu wawe hivyo; kazi yao muhimu ni kutii na kumngojea Mungu aweze kubadilisha hali zao kwani maisha yao yameratibiwa naye. Hali hii hufanya wafikie kiwango cha ung'amuzi potoshi hivi kwamba hawatambui kuwa wananyanyaswa na kwa hivyo hawatetei hali yao kuwa bora kwani huamini ni majaliwa au kudura ya Mungu.

Katika riwaya ya *Asali Chungu,* dini inatumiwa na wanajamii kama pahali pa kujificha na kujifanya kumkaribia Mungu ilhali wanatenda maovu yasiyohusishwa na dini au yasiyomfurahisha Mungu. Kwa mfano, Zuberi katika sala ya alfajiri anaonyesha ukarimu katika mwezi wa kutoana mashimoni (ikimaanisha mwezi wa kusaidia maskini). Hali hii inadhihirisha dhana ya Marx kuwa dini hutumiwa kuhalalisha maovu ya watawala ili kuendeleza itikadi tawala na hivyo pia kuthibitisha mtazamo wa Althusser kuhusu itikadi kuwa dini ni kigeu kikuu cha kuendeleza itikadi tawala. Althusser (1981) anasema kuwa kuna asasi tofauti za utawala ambazo huendeleza itikadi za kitawala, asasi hizo ni elimu, dini, mahakama, vyombo vya habari, vyama vya kisiasa na vyama vya wafanyakazi kati ya nyinginezo. Asasi hizi za utawala huhalalisha mifumo ya kiutawala iliyopo ama kwa njia za ukubalifu au kwa matumizi ya nguvu kama vile jeshi na polisi. Wahusika kama Mzee Zuberi anamnajisi Semeni (uk.11) na hakuna sheria inayochukuliwa au hata kufikishwa mahakamani. Isitoshe, Mzee Zuberi anamwagiza Mzee Omari amletee binti yake ili washiriki kitendo cha ngono. Ingawa hii inaonekana wazi kuwa ni ukiukaji wa haki za mtoto wa kike, Mzee Zuberi hayajali haya maana anajiona kuwa yuko juu ya sheria. Kupitia kwa Mzee Zuberi, mwandishi anaonyesha tajiri kama mwenye haki ya kutenda lolote lile mradi atimize haja zake na sheria haizingatiwi bali hutumiwa kuhalalisha matendo ya tabaka tawala na kuharamisha matendo ya tabaka la chini linapojaribu kijinasua.

Kuhusu haki ambayo ni hali ya kuwa na usawa kwa kila binadamu mtunzi anaonyesha kuwa mnyonge anaonekana kunyimwa haki zake. Kwa mfano walalamikaji waliofika kwa Bwana DC ili kuwasilisha malalamiko yao hawahudumiwi na wanapuuzwa ilhali ni haki yao kuhudumiwa licha ya kwenda

hapo mara nyingi na kutembea kwa mwendo mrefu. Aidha, Bwana DC anasawiriwa kama mwakilishi wa serikali dhalimu ya kimwinyi na hutumiwa kuendeleza itikadi ya watawala. Watu wakimuona tu wananyamaza na kunyenyekea ati ni utiifu lakini kwa hakika ni uendelezaji wa itikadi tawala ya kimwinyi. Hivyo, asasi za utawala kama vile Bwana DC ni vigeu nyamazishi vya kuendeleza itikadi tawala ya kimwinyi.

### 3.1.1 Itikadi ya Mwandishi

Mohamed katika riwaya ya *Asali Chungu* anaongozwa na itikadi ya mapinduzi ya marekebisho ya asasi za mfumo mzima wa umwinyi. Anaonyesha kuwa kwa kurekebisha asasi za itikadi ya kimwinyi kutafanya hali kuwa bora kwa watu wote. Itikadi hii inajitokeza kutokana na marekebisho anayoridhia yafanywe katika asasi za kimwinyi kama mfumo wa kiuchumi, matabaka, elimu, utamaduni, dini, mfumo wa kuumeni, asasi za utawala, na ndoa na mapenzi. Mwandishi anaamini kuwa marekebisho yakifanywa katika mifumo na asasi hizi na watu wakifuata dini na maadili maisha yatakuwa bora.

## 3.2 Itikadi katika *Kiza katika Nuru*

Itikadi kuu inayojitokeza katika *Kiza katika Nuru* ni ya kibepari. Itikadi hii inajidhihirisha kwa makali yake ya ukandamizaji kupitia vipengele kama vile mfumo wa kiuchumi, utabaka, elimu, utamaduni, mfumo wa kuumeni, ndoa na mapenzi, dini, maadili na asasi za utawala. Mfumo wa kiuchumi unaojitokeza katika riwaya hii ni wa kibepari ambapo kuna kumiliki makampuni makubwa na kunyanyasa wafanyakazi. Riwaya inaonyesha kwamba Bwan Juba ana cheo serikalini na ni tajiri mwenye kumiliki makampuni ambayo ameajiri watu wengi akiwamo mtoto wake Mvita. Hata hivyo, haridhiki na utajiri huo na anataka kuwa tajiri zaidi hali ambayo inamfanya apingane na mtoto wake, Mvita. Mvita anaona kuwa babake anakosea kwa kuwanyanyasa raia na kujitajirisha yeye na aila yake. Bwan Juba haelewi ni kwa vipi Mvita, ambaye amemsomesha hadi Chuo Kikuu kwa kutarajia kuwa ndiye mrithi wake, anageuka na kuanza kumpinga. Juba anajaribu awezavyo kuhodhi mali kwa njia za magendo kwa kuwatumia vijana kama vile Baker ili aendelee kujilimbikizia mali. Mvita anapotofautiana na Bwan Juba anafutwa kazi kwa madai ya uchochezi pamoja na wafanyakazi wengine saba akiwamo Salma mpenzi wake. Aidha, anafukuzwa nyumbani na kuambiwa kuwa asirudi kabisa (uk.25). Bwan Juba yu radhi kupoteza mwanawe mradi ahifadhi mali na tabaka lake kifedha kudhihirisha nguvu ya mfumo wa kibepari.

Mtunzi wa riwaya hii anaonyesha kuwa utabaka ni adui mkubwa hasa katika mfumo wa kiuchumi wa kibepari ambapo utu na ubinadamu hauzingatiwi. Mvita anapofutwa kazi anabakia kuwa tabaka la chini kwa kulazimika kwenda kufanya kazi kama kuli na kulima mihogo hali inayomfanya aweze kupata nafasi ya

kutangamana na maskini wengine wa ulimwengu. Matabaka yanajitokeza kama kigeu cha kiitikadi kwani Bwan Juba anahalalisha vitendo vyake viovu kwa kuhifadhi utabaka kama vile wizi wa mali ya umma ili atajirike zaidi. Bwan Juba anamfukuza Kudura (mkewe) kwa kutoafikiani na tabaka lake jipya, anamfukuza Mvita kwa kutokubaliana naye kuhusu unyanyasaji wa watu walio wengi na kujitajirisha yeye mwenyewe na familia yake na baadaye kumuua anapokuwa kizingiti katika azma yake ya kutaka kuwa mbunge.

Mara nyingi mifumo ya kiuchumi hufungamna na elimu na kazi. Watu ambao hawana elimu hulazimika kufanya kazi za hadhi ya chini za kutumika na kuhudumia watu kama watumwa wao kwa kutii na kufuata lolote waambiwalo. Kinyume na hili ni kwamba watoto wa matajiri na mabepari hupata elimu nzuri kama vile Mvita jambo linalomfanya kupata kazi nzuri. Hata hivyo, anatofautiana na babake na kufutwa kazi hali inayomfanya kutafuta kazi ambazo zilikuwa maarufu kule mijini za ukuli na uchukuzi (Njogu, 1997:26). Kupitia kazi yake ya ukuli na uchukuzi Mvita anatangamana kwa urahisi na wafanyakazi wenzake na kuendeleza harakati za ukombozi. Watoto wa matajiri wanapata elimu na kazi nzuri kama ambavyo Bwan Juba alivyompeleka Mvita chuoni na kumpatia wadhifa mkuu kazini ili kumtayarisha kumrithi. Hali hii inadhihirisha mtazamo wa Althusser kuwa elimu ni kigeu kimojawapo cha kiitikadi. Elimu hutumiwa kuwatayarisha watu kwa majukumu tofauti katika jamii zao na hivyo kuhalalisha vitendo vyao. Aidha, wale wengi mbao hawakupata elimu huuza walichonacho ili wajikimu kimaisha na kufanya kazi kama ya kuuza supu, maandazi, uji na kadhalika.

Vilevile, mtunzi anaonyesha ndoa na familia kama kigeu cha itikadi tawala ya kibepari. Katika riwaya hii familia ya Bwan Juba imekumbwa na mikinzano mikubwa kiasi cha kuishia kwa tanzia ya msururu ya mauaji jambo linalodhihirisha makali na ukatili wa ubepari. Kwanza Bwan Juba anamfukuza Mvita kazini na nyumbani, na kudai kuwa anawachochea watu ofisini kuasi uongozi wake. Baadaye Bwan Juba anamuua Mvita kwa kumuona kama kizingiti katika azma yake ya kuwa mbunge. Aidha, anamfukuza Mbishi kutokana na picha aliyoichora ukutani mwa nyumba kumdhihaki Bwan Juba kwa vitendo vyake vya magendo na wizi. Baadaye anamfukuza Kudura anapotaka kupigana naye alipomdharau na kumnyanyasa. Mambo yanayojidhihirisha katika familia na ndoa ya Bwan Jabu yanafungamana na nguvu ya mfumo wa kibepari ambapo mabepari huwa radhi kufanya lolote mradi wahifadhi nyadhifa zao. Kwa hivyo asasi ya familia inajitokeza kama kigeu cha itikadi tawala ya kibepari na hivyo kudhihirisha mtazamo wa Althusser kuhusu itikadi kuwa familia ni mojawawapo ya vigeu vinavyotumiwa kuendeleza itikadi tawala kwa kuhimiza utiifu.

Mhusika wake mkuu Bwan Juba ni tajiri maarufu, kiongozi wa serikali na shehe katika msikiti ulioko kijiji cha Maweni. Hata hivyo anashiriki magendo, wizi na udhalimu dhidi ya raia jambo linaloonyesha unafiki mkubwa wa kidini.

Mathalani, siku moja alipokuwa akitoa hotuba katika msikiti wa Maweni, na Mvita alipotaka kuuliza maswali anatolewa nje na nusura auwawe na waumini waliokuwa wametekwa na hotuba ya Shehe Juba. Kudura anateseka sana katika ndoa yake na Bwan Juba lakini kwa sababu za kidini anavumilia mengi. Anapozinduka na kupigania haki zake anafukuzwa. Kudura anaungama kimoyomoyo kuwa Mungu ni mkubwa, Mungu anajua yote (uk.75). Kupitia kwa Kudura, mtunzi anaonyesha namna dini inavyoweza kumpumbaza mtu asiuone ukweli kuhusu maisha yake kama anavyobainisha Marx (1973). Aidha, Althusser (1981) anasema kuwa asasi za utawala zinazoendeleza itikadi tawala kama vile mahakama, vyombo vya habari, watawala, polisi na jeshi huhalalisha mifumo ya kiutawala iliyopo ama kwa njia za ukubalifu au kwa matumizi ya nguvu kama vile jeshi na polisi. Asasi hizi za kiutawala zinatumiwa kuzima juhudi za wanyonge wasitetee haki na usawa. Nao utawala na asasi zake hujinasibisha na tabaka lenye nguvu za kiuchumi.

Katika *Kiza katika Nuru*, askari kama asasi ya utawala wanatumiwa kuwashika Kudura, Mbishi na Salma na kuwashitaki kwa mauaji ya Bwan Juba na Mvita. Kudura anajiua mbali na gereza kulindwa na askari. Askari wanatumiwa na utawala kuwakamata raia na kueneza hofu miongoni mwa raia ndiyo maana kina Mvita wanafanya siasa kichinichini. Walikuwa wanajificha misituni na kula viapo vya kuendeleza mapambano. Askari anapouawa, askari wanaenda kumshika Salma kwa nguvu na kumshtaki. Hii inadhihirisha mkabala wa Althusser kuhusu itikadi kuwa vyombo vya nguvu kama askari na jeshi huweza kutumiwa kuwanyamazisha watu wanaopinga itikadi tawala.

Mahakama nayo inatumiwa kama asasi ya kulinda masilahi ya mabepari na kuonekana kudhulumu wanyonge kwa kutowalinda na hivyo watu kukosa imani na asasi hii. Kwa mfano wanyonge kama vile Mbishi, Kudura na Salma ndio wanaoshikwa na kushitakiwa ilhali wenye nguvu na mamlaka kama Bwan Juba wanaachwa huru licha ya kufanya maovu kama vile ufisadi, magendo, mauaji na wizi. Hali hii inafungamana vizuri na mkabala wa Althusser kuwa mahakama na sheria ni asasi zitumiwazo na watawala kuendeleza itikadi ya kitawala. Ni vigeu vya kiitikadi kwani vinatumiwa kuhalalisha maovu yanayoendelezwa na mfumo wa utawala wa kibepari.

Kuhusu vyombo vya habari, mtunzi wa *Kiza katika Nuru* anaonekana kuvipa uwezo wa kupitisha ujumbe. Kwa mfano, Bwan Juba anapoelekea kumuona Kudura ana gazeti garini ambalo limeandikwa *The Truth*. Katika gazeti hilo anaona katuni iliyokuwa na picha ya chatu mkubwa mwenye kinywa wazi aliyeandikwa “THE HAVE”, akifukuza kipanya kidogo kilichoandikwa “THE HAVE NOT”. Pia, kuna katuni ya chatu mkubwa anayengojea kuwameza wote wawili imeandikwa “THE POWER”. Inavyodhihirika ni kwamba mtunzi wa riwaya hii anaonyesha namna vyombo vya habari vinavyotumika kama asasi ya kuendeleza itikadi tawala (taz. Althusser). Ingawa katuni inawabeza wenye mali na wasio na mali kwamba

hawaelekei popote kwani wote wanatafuta mamlaka na ukubwa tu hivyo watamezwa na chatu lilioandikwa "THE POWER", Bwan Juba anacheka na kudharau ujumbe huo (uk. 112).

### 3.2.1 Itikadi ya Mwandishi

Itikadi ambayo Mohamed anairidhia katika *Kiza katika Nuru* ni ya mapinduzi ya nguvu. Mapinduzi ya aina hii huweza kutokea kama watawala hawazingatii hali mbalimbali za kijamii au kutokana na kupuuza hali hizi (Njogu, 1997). Katika riwaya ya *Kiza katika Nuru*, mtunzi anaonyesha kuwa mapinduzi yanayotokea yalikuwa ni jambo la lazima kwani utawala unaowakilishwa na Bwana Juba ulishindwa kujirekebisha licha ya kufahamu udhaifu wake. Kwa kuwa utawala wenyewe uliunga mkono ukandamizaji mapinduzi ya nguvu yalikuwa ndiyo njia ya pekee ya kujikomboa na kujinasua kutokana na utawala wa kibepari uliokithiri. Mohamed anaonyesha namna ambavyo Mvita anamfahamisha Bwan Juba maovu yake naye Bwan Juba badala ya kuyarekebisha anamfuta Mvita kazi na kumfukuza nyumbani pamoja na wafanyakazi walioonekana kumuunga mkono kama Salma.

Mohamed katika *Kiza katika Nuru* ana itikadi kuwa shughuli ya mapinduzi ni hatari inayohitaji umakini na uangalifu mkubwa na maandalizi ya muda mrefu. Mhusika mkuu Mvita anayemsawiri kama kiongozi wa mapinduzi amesawiriwa kama msomi wa Chuo Kikuu kwa hivyo anaelewa vyema masuala ya jamii yake. Mvita anashiriki katika kuwazindua watu, akiwamo mama yake. Bwana Juba anapotaka kupigania kiti cha ubunge anamuona Mvita kama kikwazo kikubwa kwake na anaamua kumuua jambo analolifanikisha kwa kumtumia Shazia anayejifanya rafiki wa Mvita na Salma. Mtunzi anaonyesha kuwa juhudi za mapinduzi hukumbwa na usaliti mkubwa hasa pale Mvita anapouawa na hivyo mapinduzi hupaswa kuandaliwa vyema.

## 3.3 Ulinganishi wa Itikadi katika *Asali Chungu* na *Kiza katika Nuru*

Msimamo wa Mohamed sio mmoja na tengemano bali unabadilika kulingana na kipindi tofauti cha utunzi wake. Katika riwaya hizi Mohamed anaonyesha mabadiliko, kwa mfano katika *Asali Chungu*, watu wa tabaka la chini wanaungana mara moja bila kufunzwa na kuamua kuleta mapinduzi. Tabaka hili la chini halielimishwi wala kufahamishwa na yeyote kuhusu hali zao, aidha viongozi wao hawaonyeshwi kuwa ni wenye elimu au fikra pevu inayowasaidia kuwazindua. Aidha, katika *Asali Chungu* kuna mgawanyiko na mikinzano katika tabaka la chini kiasi cha kutoaminika kwamba wanaweza kubadilisha hali yao kwani hata hawamfahamu adui yao ni nani. Tabaka hili halijapevuka kiasi cha kufanikisha mapinduzi. Kwa upande wa *Kiza katika Nuru* mtunzi anaonyesha kwamba lazima tabaka la chini liwe na urazini wa kitabaka ambao huchukua muda mrefu. Pia, tabaka hili la chini huwa na changamoto na hatari nyingi ili kufanikisha mapinduzi ya

kuling'oa tabaka tawala. Yaani, kuondoa utabaka sio jambo la sadfa, la kubahatisha au la kighafla tu bali ni jambo gumu lenye kuhitaji matayarisho kabambe, ya muda mrefu, umakini na upevu wa fikra. Katika *Kiza katika Nuru* anaona kwamba mapinduzi ya nguvu lazima yatokee ili kung'oa matabaka katika jamii.

Itikadi ya Mohamed kuhusu ndoa na familia katika *Asali Chungu* na *Kiza katika Nuru* pia ni ya kimapinduzi ingawa inatofautiana kidogo. Kwa mfano, Bwana Zuberi katika *Asali Chungu* hamfukuzi mkewe Amina na wanaishi naye nyumba moja kuonyesha itikadi yake ya mapinduzi ya kurekebisha mfumo lakini katika *Kiza katika Nuru* Bwan Juba anamfukuza mkewe Kudura baada ya kupigana naye hadharani na wanawe Mvita na Mbishi hivyo familia yake inasambaratika. Hali hii inazidi kudhihirisha itikadi yake ya matumizi ya nguvu na mapambano ya moja kwa moja katika kubadilisha mambo. Kupitia ndoa ya Kudura na Bwan Juba, mwandishi anaonyesha ndoa na familia kama mojawapo ya asasi za itikadi ya kibepari. Jambo hili linaungana vizuri na mawazo ya Althusser (1981) kwamba familia na ndoa ni kigeu kimojawapo cha kiitikadi kinachotumiwa kuhalalisha udhalimu. Ni kwa kupitia ndoa ambapo Juba anaona ana haki ya kumtesa mkewe Kudura. Hali hii ni tofauti na ile inayodhihirika katika *Asali Chungu* ambapo ingawa ndoa ya Zuberi na Amina imekumbwa na uasherati usio na kipimo lakini inaendelea. Aidha, ndoa kati ya Dude na Shemsha imejaa uasherati lakini hawatalikiani.

Kinyume na ilivyo katika *Asali Chungu*, mtunzi anaonyesha kubadilisha msimamo wake kuhusu dini. Kwanza, anaonyesha dini kama dhana ambayo inahitaji muumini kujisaili na kujiuliza maswali mwenyewe kama inaafiki mahitaji ya jamii ama hapana. Tunamuona mhusika mkuu Mvita (uk. 183) akijiuliza maswali mengi na kuona dini kama imejawa na unafiki tu. Anaonyesha dini kama asasi hatari, yaani badala ya kumletea mwanadamu wokovu na amani inamletea madhara kwa kumpumbaza asiuone ukweli unaomzunguka ili ajikomboe. Aidha, kwa kumsawiri Mvita msikitini na kufanya mazingira ya msikiti kuwa uwanja wa makabiliano, mtunzi anaafiki kwamba dini sio takatifu tena; dini kama pahala pa kuabudu hapaheshimiwi tena. Inavyoelekea ni kwamba, itikadi yake kuhusu dini na pahali patakatifu inaonekana kubadilika. Katika *Asali Chungu* hajaonyesha kama dini iliwapumbaza wahusika kiasi cha kutoona ukweli wa mambo au pahala pa ibada kuwa na fujo na makabiliano. Jambo hili linatokana na kubadilisha itikadi yake ya kimapinduzi; katika *Asali Chungu* ni mapinduzi ya kurekebisha wakati katika *Kiza katika Nuru* itikadi yake ni ya mapinduzi ya makabiliano ya moja kwa moja.

Mohamed anaamini kuwa asasi za utawala zimepewa nafasi kubwa kuendeleza na kudumisha itikadi ya kibepari iliyotawala kipindi alichoandika riwaya ya *Kiza katika Nuru*. Asasi hizi zinatumiwa kueneza imani za tabaka dogo linalotawala na kuwafanya wanaonyanyaswa kutokuwa na matumaini ya kubadilisha hali zao kuwa bora. Kama Althusser (1981) anavyosema kwamba itikadi huweza kuelekezwa katika nguvu kama vile jeshi, polisi na mahakama au kwa kutumia vyombo vya

kiitikadi kama dini, elimu, utamaduni na vinginevyo. Hata hivyo, licha ya kuisawiri hali hii msimamo wa Mohamed umebadilika kuhusu asasi hizi kwani anaonyesha kuwa zinahitaji kufanyiwa mapinduzi ya nguvu na kung'olewa kabisa; sio kurekebishwa tu kama ilivyo katika *Asali Chungu*. Kwa mfano, Kudura anazinduka na kupigana na Bwan Juba hadharani, Mvita anakabiliana moja kwa moja na babake msikitini, Salma anajitetea sana mahakamani na kuna ishara kuwa ataachiliwa, na mwishowe Bwan Juba anauawa na mapinduzi kufanyika. Kwa hivyo, Mohamed anaonekana kubadilisha itikadi yake ya hapo awali kuwa asasi hizi zirekebishwe ili zisitumike tu kuyalinda maslahi ya mabepari bali zifanyiwe mapinduzi ya nguvu na ziondolewe kabisa.

Mtunzi kupitia gazeti la *Truth* ambalo Bwan Juba analitumia kujipepea anaonyesha kuamini kuwa jukumu la vyombo vya habari sio tu kueneza ukweli bali itikadi za tabaka tawala. Hivyo anakubaliana na Althusser (1981) anayesema kuwa vyombo vya habari ni mojawapo ya vifaa vinavyotumiwa na tabaka tawala kueneza uongo na itikadi za kitawala ili waendelee kudumisha matabaka. Aidha, katika shughuli za kuendeleza mapinduzi, Maharamu, mhariri wa gazeti hilo, alikuwa hapatikani na hatimizi miadi kila wakipanga wakutane na Salma. Jambo hili linaonyesha namna vyombo vya habari na wanahabari wanavyotumiwa na tabaka tawala kutosema ukweli na kueneza propaganda za kiutawala ili kuficha maovu wanayotenda, hivyo ni washirika wa tabaka tawala katika ukadamizaji.

Mohamed katika *Kiza katika Nuru* anaonyesha namna asasi za utawala kama vile polisi na mahakama zinavyotumiwa kudhibiti hali na kulinda maslahi na matakwa ya tabaka tawala kuhusu itikadi (taz. pia Althusser, 1981). Anaamini kuwa asasi hizi zinatumiwa kama vyombo vya ukadamizaji. Mathalani, polisi wanatumiwa kumshika Salma na kumshitaki, Kudura anashikwa na kufunguliwa mashtaka na anajiua akiwa rumande, ilhali Bwan Juba hakushikwa kwa kushiriki mauaji ya Mvita kati ya maovu mengine. Mohamed anaamini kuwa mapinduzi ya nguvu yaliyopangwa vyema ndiyo hufanikisha juhudi za ukombozi kama Althusser (1981) anavyosema kwamba vyombo vya kiitikadi vya serikali ni vingi mno; kuna vile vinavyotumia nguvu kama jeshi, polisi na mahakama na vile vinavyotumia itikadi kuwafanya watu wanyamaze na wasitetee hali zao duni na kuendeleza itikadi tawala.

Aidha, ndoa, familia na dini zimeonyeshwa kama asasi za kuendeleza itikadi za utawala wa kibepari kwa wakati huu. Mathalani, Bwan Juba anataka Mvita aendeleze utabaka, anapokataa anafukuzwa kazi, kwenye nyumba na mwishowe kuuawa. Naye Kudura ananyanyaswa katika misingi ya ndoa na dini kwa muda mrefu kabla ya kujitokeza na kutetea utu na ubinadamu wake na mwishowe kumuua Bwan Juba. Mtunzi katika riwaya zake hizi mbili anadhihirisha mabadiliko ya kiitikadi. Katika *Asali Chungu* anaonesha kwamba Zuberi na Amina ni wanafiki na hawadanganyiki na dini. Pia anaonesha kwamba Dude, Baya na wahusika wengine

wa tabaka la chini hawatetei hali zao. Zuberi na Amina wanashiriki kuwakandamiza zaidi Biti Daudi, Bushiri na wengineo lakini hawazinduki. Hali yao ni ileile hata mapinduzi yanapofanywa hawaonyeshwi kushiriki katika juhudi zozote za ukombozi au kubadilisha maisha yao kuwa bora. Hivyo basi, itikadi ya mtunzi katika *Asali Chungu* inataka mapinduzi ya marekebisho ya asasi za mfumo mzima wa umwinyi wakati katika *Kiza katika Nuru* itikadi yake inasisitiza mapinduzi ya nguvu; asasi zote zinazoendeleza itikadi tawala ya kibepari zing'olewe kabisa wala sio kufanyiwa marekebisho.

**4.0 Hitimisho**

Katika makala hii tulidhamiria kuonyesha itikadi zinazojitokeza katika riwaya za awali za S.A Mohamed ambazo zinawakilishwa na riwaya ya *Asali Chungu* na *Kiza katika Nuru*. Lengo letu likiwa ni kudhihirisha kuwa itikadi ni dhana badilifu na nyumbufu na hivyo mtazamo wa mtunzi ni changamano. Ili kuonyesha unyumbufu wa dhana ya itikadi makala hii imetumia dhana za itikadi kwa mujibu wa Marx, Althusser na Gramcsi. Tumeona kuwa itikadi huweza kuwa ung'amuzi potoshi (Marx), ukubalifu na ukawaida (Gramsci) au dhana za kitawala zinazoendelezwa na vyombo vya taifa na vyombo vya utawala (Althusser), na hivyo dhana ya itikadi ni changamano.

Katika riwaya ya *Asali Chungu* itikadi tawala ni ya kimwinyi. Itikadi hii imejitokeza kupitia vigeu kama vile mfumo wa kiuchumi, matabaka, elimu, ndoa, mfumo wa kuumeni, utamaduni, asasi za sheria na utawala na dini. Tumeona kuwa vigeu hivi sio dhana za kawaida kama ambavyo wahakiki wengi huchukulia, bali ni vigeu vikuu vya kuendeleza itikadi kuu ya tabaka tawala la kibwanyenye ili kuhalalisha mfumo huo. Aidha, itikadi ya mtunzi nayo hujitokeza katika kazi yake kupitia maudhui, wahusika na mtindo wa kazi nzima ya fasihi. Katika riwaya ya *Asali Chungu* itikadi ya mtunzi inayojitokeza ni ya mapinduzi ya marekebisho ya mifumo ya kiuchumi, kuumeni, utamaduni, ndoa, elimu, dini, sheria na asasi za utawala. Anaonyesha kuwa mifumo hii ikirekebishwa na wahusika wakijirekebisha kitabia na mienendo, hali inaweza kuwa bora kwa jamii nzima. Tumeonyesha kuwa ingawa mwishoni mwa riwaya anasawiri aina ya mapinduzi ambapo kina Zuberi wanauawa, hata hivyo mapinduzi haya yamecheleweshwa, viongozi wake hawajaandaliwa vilivyo na hivyo yanaonekana kupachikwa tu. Hivyo mtunzi anaafiki itikadi ya mapinduzi ya marekebisho kupitia maudhui aliyojadili, namna alivyowasawiri wahusika wake na mtindo mzima wa kazi yake. Haya yote yanaonyesha kuwa itikadi ni dhana changamano na kwa sababu mtunzi huelekezwa na itikadi fulani katika kazi yake basi itikadi ni dhana badilifu na nyumbufu na msimamo wa mtunzi ni changamano.

Katika riwaya ya *Kiza katika Nuru* itikadi kuu inayojitokeza ni ile ya kibepari. Itikadi hii imejitokeza kupitia vigeu kama vile mfumo wa kiuchumi wa kibepari,

utabaka, elimu, dini, ndoa na familia, mfumo wa kuumeni, sheria na asasi za utawala. Vigeu hivi vya kiitikadi ya kibepari vimejitokeza kwa makali mno, kwa mfano mfumo wa kiuchumi na utabaka unasababisha misururu ya mauaji, elimu kutumiwa kuweka watu katika matabaka tofauti, na dini kutumiwa kuwapumbaza watu na kuhimiza utiifu. Aidha, ndoa na familia kutumiwa kuendeleza utiifu, mifumo ya kuumeni kutumika kama sehemu ya kuendeleza itikadi tawala, na sheria na asasi za utawala kama jeshi na polisi kutumiwa kunyamazisha watetezi wa haki na kulinda maslahi ya mabepari. Imedhihirika kuwa itikadi ya mtunzi katika *Asali Chungu* na *Kiza katika Nuru* ni tofauti. Itikadi hiyo imebadilika kutoka mapinduzi ya marekebisho katika *Asali Chungu* hadi itikadi ya mapinduzi ya matumizi ya nguvu katika *Kiza katika Nuru*. Hivyo basi, mielekeo na mitazamo ya mwandishi ni changamano kuliko ilivyofikiriwa hapo awali.

## Marejeleo


Achebe, C. (1988). Hopes and Impendiments: Selected Essays. London: Heinnemann.

Althusser, L (1981). Ideology and Ideological State Apparatuses katika *Lenin and other essays.* Mtafs. B. Brewster. London: New left Books.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert.* Dar es Salaam: TATAKI.

Derrida, J. (1976). *Of Grammatology and Writing and Difference*. Mtafs. G. C. Spivak. Baltmore: John Hopkins.

Gramsci, A. (1985). *Selections from Cultural Writings, 389*-390. Katika D. Forgas and G. Nowel-Smith (Watafs.). London: Lawrence and Wishart.

Hegel, G. (1977). *Phenomenology of Spirit*: Katika A.V Miller (Mtafs.). Oxford: Oxford University Press.

Hough, G. (1966). *An Essay on Criticism*. London: Redwood press.

Marx, K. na F. Engels. (1973). *On Literature and Art*. New York: International General

Marx, K na F. Engels. (1977). *The German Ideology.* London: Lawrence and Wishar

Mbatia, M. (1997). Commitment in the Swahili Novel: An Appraisal of the Works of Said

Ahmed Mohammed. katika D. P. B Massamba and Mulokozi M. M. (Wah.) *Kiswahili Vol. 60*. Dar-es-Salaam: TUKI.

Mbatiah, M. (1999). The Origin and Development of the Swahili theses novel in Tanzania Tasnifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mohamed S. A. (1978) *Asali chungu.* Nairobi: Shungwaya.

Mohamed S. A. (1980). *Utengano.* Nairobi: Longhorn

Mohamed S. A. (1986). *Kiza katika Nuru.* Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi.* Nairobi: E.A E. P.

Ngara, E. (1985) *Art and Ideology in African Novel*: *A Study of the Influence of Marxism on African Writing*. London: Heinemann.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: U. O. N. Press.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: *Nadharia na Mbinu*. Nairobi: JFK.

Osore, K. (2008). Defamiliarization in the novels of Euphrase Kezilahabi and S. A. Mohamed. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Plato (1969) *The Republic*. I.A Richards (mtaf. na mhar). Cambridge: Cambridge University Press.

Rossiland, F. (1990). *Marxism and Ideology.* Oxford: Clarendon Press.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.